

Kiwanda cha samaki Tanga kuajiri Watanzania 100

Na Anna Mwikola

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imesema kampuni ya Albacora ya Hispania imekubali kuanzisha kiwanda cha kuchakata samaki mkoani Tanga.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega alisema hayo katika Bandari ya Dar es Salaam jana wakati serikali inapokea tani 50 za samaki kutoka kwenye meli ya uvuvi ya kampuni hiyo.

Ulega alipokea samaki hao alipotembelea meli hiyo yenye leseni na ithibati ya Tanzania, kwa ajili ya ukaguzi na kupokea samaki hao.

Alisema kampuni hiyo tayari imenunua ardhi Tanga kwa ajili ya mradi huo na wanatarajia kutoa ajira zisizopungua 100 kwa vijana wa Kitanzania.

Ulega alisema kiwanda hicho kitakuwa ni cha kwanza kikubwa Afrika Mashariki na ni matokeo ya sera za uwekezaji za Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema Rais Samia anataka kuona sekta binafsi inakuwa injini ya uwekezaji, biashara na uzalishaji na hilo litawezekana kwa kuacha kazi kama hizo zifanywe na sekta hiyo.

Ulega alisema kwa sasa serikali iko kwenye jitihada kukamilisha bandari za uvuvi za Kilwa Masoko na Bagamoyo ili kutanua wigo wa sekta ya uvuvi na kuongeza tija kwenye uchumi

wa bahari.

"Maana yake itakapokuwa tayari meli za namna hii zitakuwa zinakwenda kufunga gati kule kwenye Bandari ya Kilwa masoko na nyingine tunaitarajia kuijenga Bagamoyo, kwa hiyo tutakuwa tumefungua milango, sasa hivi hizi meli haziji kwa wingi kwa sababu hapa siyo eneo sahihi kwa ajili ya meli za samaki, hili ni eneo kwa ajili ya meli za mizigo ndiyo maana hatupati wengi wanaokuja," alisema.

Ulega alisema ukaguzi aliofanywa ni wa kawaida kuangalia kama makubaliano yaliyowekwa kwa mujibu wa leseni na utaratibu husika vinazingatiwa na kwamba mkataba unaitaka kampuni hiyo ikipata samaki aina tofauti na jodari wawarudishe serikalini.

Alisema samaki hao wanaporudishwa, huingizwa sokoni kwa gharama za chini hivyo kusaidia kupunguza bei ya samaki katika soko la samaki la Feri.

Mwakilishi wa Kampuni ya Albacora, Julien Erekatxo alisema amefurahishwa na ukarimu wa Watanzania na ndiyo sababu wameshawishika kuanzisha kiwanda cha kuchakata samaki mkoani Tanga.

"Na bosi wa kampuni anatarajiwa aje Tanzania Desemba 6 kwa ajili ya kutiliana saina mikataba na kukamilisha taratibu nyingine," alisema Erekatxo.

Na

V

Mk
Mic
za
wa
mir

baa
Shu
cha

mk
wa
kw
ni

* Ulega: Ubia sekta binafsi, umma * kutaimarisha kilimobiashara

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amesema kuimarika kwa ubia kati ya sekta za umma na binafsi kutakuza shughuli zinazoimarisha kilimobiashara nchini.

Ulega alisema hayo Dar es Salaam jana wakati akifungua mkutano wa 15 wa Chama cha Wachumi Kilimo Tanzania (AGREST).

Alisema mafanikio zaidi katika kilimo yatapatikana kupitia ubia kati ya sekta za umma na binafsi.

"Asilimia 65.5 ya Watanzania milioni 61 wamejiajiri kwenye sekta ya kilimo ambacho kinachangia asilimia 26 ya Pato

la Taifa (GDP) na katika Tanzania kilimo kinatoa asilimia 65 ya ajira mbali ya malighafi inayotumika viwandani," alisema Ulega.

Aliongeza: "Ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi madhubuti wa Rais Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Kilimo hatua zimechukuliwa kuhakikisha sekta binafsi inatoa mchango stahiki kwenye uzalishaji katika sekta ya kilimo."

Ulega alisema takwimu za hivi karibuni zinaonesha kilimo kimeliingizia takribani Dola za Marekani bilioni 1.4 kwa mazao yaliyouzwa nje na hivyo kuwa sekta muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa Tanzania.

Alisema kilimobiashara

na ushauri wa wataalamu vikizingatiwa kitatoa mchango mkubwa katika kukuza pato la mkulima mmojammoja pamoja na kukuza pato la taifa.

Ulega alisema mkutano huo utapata pia fursa ya kujadili namna bora ya kutatua changamoto zinazoikabili sekta hiyo zikiwamo bidhaa kuyafikia masoko, teknolojia na ubunifu, ushiriki wa vijana, upataji wa fedha, ubia kati ya sekta za umma na binafsi (PPP) na uongezaji wa thamani kwa mazao.

Mwenyekiti wa AGREST, Dk Florens Turuka alisema kilimo kinachangia asilimia 35 ya thamani ya chumi katika Afrika ambapo kilimo kinachangia asilimia 50 ya thamani ya uchumi wa dunia.

HABARI LEO UK. 7

RAIS Mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete akikabidhi cheti kwa Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Tehama (ICTC), Dk. Nkundwe Mwasaga kwa niaba ya watoa mada kuu walioshiriki katika Kongamano la Nne la Kitaaluma la Biashara na Uchumi lililofanyika jana jijini Dodoma chini ya uratibu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE). Dk. Kikwete aliyekuwa mgeni rasmi katika kongamano hilo, alikabidhi vyeti kwa kutambua mchango wa wazungumzaji hao kwenye tasnia ya Taaluma, Biashara na Uchumi. (Na Mpiga picha Wetu).

daraja hilo likikamilika litatungua tursa za kiuchumi zilizopo mkoani Tanga.

Mbunge wa Pangani na Waziri wa Maji, Jumaa Awesso alimpa salamu Waziri Bashungwa amfikishie Rais Dk. Samia kutokana na kutoa fedha za kujenga daraja hilo ambalo litakuwa ni suluhisho la kudumu kwa wananchi wa Pangani.

*^{UHURU UK 3} Kiwanda kikubwa cha kuchakata samaki kujengwa nchini

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema kufuatia sera nzuri za kuvutia uwekezaji za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, zimeanza kuleta matunda katika uchumi wa buluu.

Hali hiyo inatokana na Kampuni ya Albacora kutoka nchini Hispania kuja nchini kujenga kiwanda kikubwa cha kisasa cha kuchakata

samaki ambacho kitakuwa cha kwanza katika Ukanda Pwani ya Bahari.

Waziri Ulega amesema hayo jana wakati akifanya ukaguzi wa meli ya kampuni hiyo iliyobeba Tani 50 ya samaki wasiolengwa walioletwa na kampuni ya Albacora, bandari ya Dar es Salaam.

Alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitoa leseni kwa kampeni hiyo ya uvuvi wa samaki aina ya

jodari katika ukanda wa bahari kuu, leseni hiyo imeeleza wakipata mazao mengine ya biashara watarejesha kwa serikali.

Kwa mujibu wa Waziri Ulega, Kampuni ya Albacora imepewa leseni ya Tanzania kuvua samaki aina ya Jodari katika bahari kuu na makubaliano ni kwamba wakipata samaki mwingine tofauti na Jodari wanapaswa kuwarudisha hapa nchini.

"Leo wameleta samaki tani

50 ambao si wale waliokusudia na samaki hao wanauzwa na kupelekwa katika soko la feri. Hii itasaidia kupunguza shida na bei ya samaki katika soko hilo" alisema.

Aliongeza; "Mheshimiwa Rais anavutia zaidi sekta Binafsi kufanya kazi za uwekezaji hapa nchini uwe injini ya uwekezaji, biashara na uzalishaji na ndio maana kampuni ya Albacora wako tayari kuwekeza hapa nchini"

Alisema "Kampuni imeshanunua eneo katika mkoa wa Tanga kwa ajili ya kujenga kiwanda hicho kitakachotoa ajira ya moja kwa moja kwa vijana wa kike na kiume wasiopungua 100,"

Hivyo, alisema kuna jitihada kubwa za Rais, Dk. Samia za kujenga bandari ya uvuvi ya Kilwa Masoko kutawezesha meli nyingi kubwa kama za Albacora kutoka nje ya nchi kutia nanga hapa nchini.

UHURU

MAONI YA MHARIRI

Hongera Wizara ya Mifugo na Uvuvi kutekeleza maono ya Rais Dk. Samia

JANA Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amefanya ukaguzi wa meli ya kampuni ya Al Bacora kutoka nchini Hispania inayofanya shughuli za uvuvi katika ukanda wa bahari kuu.

Meli hiyo ilitia nanga katika Bandari ya Dar es Salaam na kutoa mwelekeo wa maono ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika kutekeleza sera ya uchumi wa buluu.

Rais Dk. Samia amekuwa mstari wa mbele kuvutia wawekezaji katika sekta mbalimbali nchini, juhudi hizo zimeanza kuleta matunda kwa wawekezaji wengi kuja hususan eneo la uchumi wa buluu.

Kitendo cha Kampuni ya Albacora kutoka nchini Hispania kuja nchini kujenga kiwanda kikubwa cha kisasa cha kuchakata samaki ambacho kitakuwa cha kwanza katika Ukanda Pwani ya Bahari mkoani Tanga ni jambo bora.

Hali hiyo inatokana na mipango bora ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi chini ya Waziri Abdallah Ulega kutekeleza malengo na maono ya Rais Dk. Samia kuifanya sekta ya uvuvi kuwa chanzo kikuu cha mapato ya nchi.

Ujio wa meli hiyo iliyobeba Tani 50 ya samaki wasiolengwa walioletwa na kampuni ya Albacora ni mafanikio makubwa kwa serikali kwa kuwa imeonyesha kwa vitendo dhamira ya serikali kuleta maendeleo.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitoa leseni kwa kampuni hiyo kufanya uvuvi wa samaki aina ya jodari katika ukanda wa bahari kuu, leseni hiyo imeeleza wakipata mazao mengine ya samaki wanapaswa kurejesha serikalini.

Kwa mujibu wa Waziri Ulega, Kampuni ya Albacora imepewa leseni ya Tanzania kuvua samaki aina ya Jodari katika bahari kuu na makubaliano ni kwamba wakipata samaki mwingine tofauti na Jodari wanapaswa kuwarudisha hapa nchini.

Tunaamini huu ni mwanzo na safari ya Rais Dk. Samia kuifanya sekta hiyo kubwa bora itaendelea na kutoa mwelekeo bora na wenye mafanikio makubwa.

Jitihada kubwa za Rais, Dk. Samia za kujenga bandari ya uvuvi ya Kilwa Masoko kutawezesha meli nyingi kubwa kama za Al bacora kutoka nje ya nchi kutia nanga hapa na kukuza uchumi wa nchi.

Hivyo, hongera Waziri Ulega kwa kuwa mstari wa mbele katika kuleta maendeleo na kutekeleza maono ya Rais Dk. Samia kupitia uchumi wa buluu.

Uhuru Publications Limited (UPL)

S.L.P. 2072, Dodoma.

Ofisi Ndogo ya Makao Makuu Dodoma; Mtaa wa Makongoro Area C Chumba cha Habari:

+255-784 - 414194, 0784 - 446797

email: uhuruvijijini@gmail.com

Mkurugenzi Mtendaji Mkuu:	0655 - 355810
Naibu Mhariri Mtendaji:	0784 - 599717
Mhariri Mkuu:	0784 - 414194
Mhariri wa Habari:	0784 - 446797
Mhariri wa Michezo:	0718 - 611700
Idara ya Siasa na Habari:	0713 - 363337

IDARA YA BIASHARA

Meneja Biashara:	0754 - 313140
Meneja Matangazo	0765 - 142207
Meneja Uzalishaji na Mauzo:	0683 - 378522

RADIO UHURU FM (PMCL)

uhurufmnews@gmail.com

Kaimu Mkurugenzi Uhuru FM	0765- 383757
Kaimu Mhariri Mkuu Uhuru FM:	0713 -248640
Meneja masoko Uhuru FM:	0715 -584 150

Ulega for bolstering of agribusiness as global and peri-urban populations rise

By Guardian Reporter

TANZANIANS must take very seriously business activities that support agriculture (agribusiness) primarily because of increasing opportunities in those activities, because of global rise in urban and peri-urban populations and their population is steadily rising. Tanzania's population stood at 43.6 million (2012) and at 61,741,120 (2022).

Addressing the 15th Agricultural Economics Society of Tanzania (AGREST) conference in Dar es Salaam, Minister for Livestock and Fisheries Abdallah Ulega, underscored this urge, saying that Tanzanians have cause to plunge into these activities because agribusinesses have grown over the years.

"The increase has been driven by growing urban and peri-urban populations (hence) the increasing demand from well-off urban consumers for different, higher quality and often high-value products and services," he said.

Besides, the Tanzanian government has taken initiatives and policies to foster agribusiness resilience.

He explained that agribusiness covers all activities ranging from production, processing, packaging, distribution to consumption of agricultural products. "It also includes related services (supplying of inputs such as fertiliser, seed, breeds and equipment) and provision of advisory and extension services to agriculture."

On initiatives and policies taken by the government, Uledi said policies and regulations have been streamlined to enhance resilience in agribusiness. This has included lifting up of food crops export bans; removing restrictions of where farmers can sell crops and livestock products without prejudice and allowing importation of specialised inputs for production and processing.

He further said, the government

and cold storage facilities and other common use facilities for processing perishable produce to ensure agribusiness value-chains covering crops, livestock and fisheries products are resilient.

In partnership with the private sector, he said, the government is working to expand international market access for agricultural produce, livestock and fisheries products.

The government has significantly increased its investment in agriculture, livestock and fisheries research and development, he said, adding that the government has embraced digital technology to improve agriculture, livestock and fisheries sectors. Further, he explained, Tanzania has adopted climate-smart agricultural practices, including drought-resistant crops, sustainable land management and promotion of climate-resilient livestock breeds.

The government's ambitious Agenda 10/30 initiative aims to attain a 10 percent annual growth rate in the agriculture sector by the year 2030. The 2022/23-2026/27 Livestock Transformation Plan, the minister said, sets out livestock sector investment areas.

He also urged Tanzanians to realise that developments are occurring in logistics, storage, transport, wholesale, retail and food services, with fundamental and rapid changes in structure, conduct, and performance in agribusiness value chain nodes.

"These developments provide new opportunities for farmers to increase their income, food security and nutrition and improve access to productivity-enhancing inputs and services."

The Chairman of AGREST, Dr Florens Turuka, told the conference that agriculture accounts for 35 percent of the value of economies in Africa and makes up to 50 percent of the value of the world economy.

to enhance the local government collections and tax fairness and ultimately further grow the tax base," he said.

Tanzania to reap more from deep sea fishing vessel

By LEONARD KONDOBOLE

TANZANIA is set to reap more from a large fishing vessel registered in the country to operate in its Exclusive Economic Zones (EEZ).

The vessel which sails under a Tanzanian flag christened Albacora is also set to establish a fish processing and packaging plant in Tanga Region with the aim of widening the market of the marine resources.

Minister for Livestock and Fisheries, Mr Abdallah Ulega yesterday received the fishing vessel with 50 tonnes of fish caught in deep sea with the aim of inspecting any deviation.

He said that the fishing vessel will contribute to increased fish supply, lowering market prices and serving as an example of sustainable fishing practices.

The minister said the company has acquired land for the construction of the processing and packaging plant.

Under the issued license, Ulega said, the (Albacora) is required to fish specific type of fish, and any deviation must be transparently disclosed to the government.

He said, "Albacora have demonstrated responsibility by returning non-specified fish to the government to stabilise fish prices in the local market."

Since Albacora began fishing in our country's deep-sea waters, Minister Ulega stated that "there have been no instances of the company violating the laws and regulations set forth."

"Thanks to the favourable investment policies set forth by the sixth-phase government and the effective leadership of President Samia Suluhu, Albacora has been persuaded to invest in the country by establishing a fish processing plant.

He further said with the completion of Bagamoyo and Kilwamasoko ports, challenges in unloading non-food cargo will be addressed.

The Albacora representative, Julen Erekatxo reaffirmed the company's plan to establish a fish processing plant in Tanzania, citing satisfaction with the government's business environment and procedures.

He said their boss is expected to come to Tanzania on December 6 this year to sign a contract with Tanzanian government so that the project in Tanga is officiated.

Mr Erekatxo said their idea is to set up a processing plant and to start operations as soon as possible by taking fish to Tanga. Albacora started working in Tanzania in 2021. For the past few years, Albacora has been